TOLEO RAHISI LA

# ITIFAKI

## Uanzishwaji wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki

*Kwa msaada wa*

TRADE MARK EAST AFRICA

EASSI
Eastern African Sub-regional Support Initiative for the Advancement of Women

# *East Africa*



TOLEO RAHISI LA

# ITIFAKI

## Uanzishwaji wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kampala, Uganda
2012

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Kuhusu EASSI | ii |
| Dibaji | iii |
| 1.0 Utangulizi | 1 |
| 2.0 Nini maana ya Soko la Pamoja? | 1 |
| 3.0 Soko la Pamoja lina Lengo gani? | 1 |
| 4.0 Ni yapi Malengo Mahsusi ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki? | 2 |
| 5.0 Ni zipi Sehemu za Itifaki? | 2 |
| 6.0 Ipi ni fasiri ya baadhi ya Sehemu za Itifaki? | 3 |
| 7.0 Zipi faida za Soko la Pamoja kwa wanawake wanaofanya biashara ya ku vuka mipaka ndani ya ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki? | 10 |
| 8.0 Vipi ni vikwazo na masuala ambayo yamekuwa yakiweka wanawake kando kwenye biashara ya kuvuka mipaka ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki? | 11 |
| 9.0 Mapendekezo | 12 |
| 10.0 Hitimisho | 13 |
| 11.0 Viambatisho:<br>Kiambatisho 1: Aina na Vyanzo vyaNyaraka muhimu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki | 14<br>15 |
| Kiambatisho 2: Hati Rahisi Ya Uasili Wa Bidhaa (SSCO) | 16 |

# Kuhusu EASSI

Asasi ya Mpango wa kuhamasisha maendeleo ya wanawake katika ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EASSI) ni asasi ya kiraia ya kikanda iliyoanzishwa mwaka 1996. EASSI ina dhima ya kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa makubaliano ya Jukwaa la Utendaji la Beijing (Beijing Platforms for Action [BPFAs]) ambacho ni chombo cha Mkutano wa nne wa wanawake uliofanyika mjini Beijing nchini China mwaka 1995. Asasi hii, ambayo imesajiliwa nchini Uganda kama asasi isiyo ya kibiashara, inafanya kazi na asasi nyingine za kitaifa katika nchi nne zikiwamo Burundi, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Somalia, Tanzania na Uganda.

### Dira yetu

Dira yetu ni kuwa na jamii yenye usawa wa kijinsia, yenye haki za kijamii, yenye amani na mendeleo.

### Dhima yetu

Dhima yetu ni kuhakikisha na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Jukwaa la Utendaji la Beijing ili kuimarsha maendeleo ya wanawake na kupigania haki za kijamii.

### Malengo yetu

- Kusimamia maendeleo ya utekelezaji wa Jukwaa la Utendaji katika ukanda, kama njia ya kuziwajibisha serikali ili zitekeleze kwa vitendo ahadi zilizowekwa Beijing
- Kupigania kuwepo kwa chombo imara cha kikanda kinachopigania kuwepo kwa haki za wanawake na usawa wa kijinsia.
- Kuhimiza matumizi na mgawo mzuri wa raslimali za Umma, na matumizi haki za afya ya uzazi na jinsia na bajeti inayojali tofauti za kijinsia.
- Kuongeza ushiriki wa wanawake katika kutoa changamoto za kupinga vyanzo vya migogoro vya kimfumo kwa kutoa njia mbadala ya kujenga amani na kuleta suluhu ya migogoro.

## Utambulisho wetu wa kipekee

**Utambulisho wetu wa kipekee upo kwenye;**

- Uwanachama na mtandao wa kikanda ;
- Usimamizi wa utekelezaji wa Majukwaa ya Utendaji ya Afrika na Beijing ndani ya ukanda wa Mashariki mwa Afrika;
- Mlengo wetu wa Kiafrika wa kupigania haki za wanawake;
- Kuwa katika nafasi nzuri ya kusema kuhusu mwendelezo wa mapambano ya kupigania usawa wa kijinsia ndani ya ukanda wa Mashariki mwa Afrika kwa kutumia muundo wa Jukwaa la Utendaji;
- Wanachama tofauti wa watu binafsi na ule wa asasi wakiwa na uzoefu na uwezo tofauti wa kimaarifa kitaifa, kikanda na kimataifa.

# Dibaji

Asasi ya Mpango wa kuhamasisha maendeleo ya wanawake katika ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EASSI) ni asasi ya kijamii ya kikanda iliyoundwa na watu binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali, miungano ya kimkakati na mitandao yenye nia ya kufanya mabadiliko ya mahusiano ya kijinsia ulimwenguni na hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kazi yetu inafuata na kuzingatia makubaliano makubwa ya kimataifa ya Jukwaa la Utendaji la Beijing (BPFA) yanayotokana na Mkutano wa nne wa wanawake uliofanyika Beijing mwaka 1995. Dira ya makubaliano hayo inathibitisha Mkataba wa kukomesha aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), na Mswaada kuhusu haki za wanawake. BPFA nayo inaendana na Azimio la Milenia na Malengo nane ya Milenia (MDG) ya mwaka 2015 ambayo ni kupambana na umaskini, njaa, maradhi, kutojua kusoma na kuandika, na unyanyasaji wa kijinsia, pamoja na kujenga ushirika wa kimaendeleo.

Mkataba wa kuunda Jumuia ya Afrika Mashariki unalitaja Soko la Pamoja la Afrika Mashariki kama hatua ya pili ambayo itasaidia kuimarisha mshikamano wa kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiteknolojia, na katika nyanja zingine kwa maendeleo yenye uwiano, ya haraka na endelevu ya Nchi Wanachama. Pamoja na hayo, Mkataba unatambua umuhimu wa wanawake na unapendekeza kuwa ushiriki wa wanawake uongezwe katika nyanja za biashara katika ngazi za uundaji na utekelezaji wa sera, uhamasishaji wa programu maalumu kwa wanawake katika biashara ndogondogo, za kati na kubwa, uondoaji wa sheria, taratibu, na vitendo vyote vinavyofanya wanawake wasiweze kupata misaada ya kifedha ikiwa ni pamoja na mikopo na kutambulika na kutoa misaada kwa vikundi vya wanawake vya kitaifa na kikanda ambavyo vimeundwa kusaidia na kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika biashara na shughuli za kimaendeleo za kijamii. Ushirikiano huu wa kikanda unaundwa na watu wenyewe na unaongozwa na soko (sekta binafsi).

Toleo hili rahisi la Itifaki, linatoa kwa ufupi vipengele vya Itifaki kwa namna inayoeleweka zaidi kwa wasomaji ili iwe rahisi kwa wanawake na waweze kuelewa. Toleo hili pia linatoa mwangaza kuhusu fursa kwa wanawake wafanyabiashara na linatoa mapendekezo kwa serikali na wadau wengine.

## 1.0 Utangulizi

Ni pamoja na mikopo kutambulika na pamoja na kusaidiwa na vyama vya kibiashara vya wanawake Jamhuri ya muungano wa Tanzania ,jamhuri ya Burundi ,jamhuri ya Kenya na jamhuri ya Uganda ni wadau wa mkataba wa uanzishwaji wa jumuiya ya afrika mashariki na wadau hawa ndio wanaoitwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika kwenye aya ya 2 ya ibara ya 2 na aya ya 2 ya ibara ya 5 ya mkataba, Nchi Wanachama zimeamua kuanzisha soko la pamoja, kama hatua ya mpito kuelekea umoja kamili ya jumuiya kwenye aya ya 2 ya ibara ya 76 ya mkataba nchi wanachama zimedhamiria kuwa uanzishwaji wa soko la pamoja utakuwa endelevu soko la pamoja la jumuiya ya afrika mashariki ni kwaajili ya kumarisha umoja wa kiuchumi kijamii kisiasa kiteknolojia na katika Nyanja zingine ili kuweka uwiano mzuri na kuleta maendeleo endelevu kwa nchi wanachama

Katika ibara za 121 na 122 , Mkataba wa uundwaji wa jumuia ya afrika mashariki unatambua umuhimu wa wanawake na unasisitiza uongezaji wa ushiriki wa wanawake katika biashara hasa katika ngaziza uundaji na utekelezaji wa sera , uhamasishaji wa programu maalumu kwa wanawake wafanya biashara ndogondogo za kati na wenye miradi mikubwa uondoaji wa sheria taratibu na mazoea vinavyowazuia wanawake wasiweze kupata misaada ya kifedha ikiwa kitaifa na kikanda ambavyo vimeundwa kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika biashara na shuguhuli za maendeleo ya jumuiya ya afrika mashariki . ushirikiano huu wa kikanda unategemea na unatakiwa ulenge watu na uendeshwe na watu na uendeshwe na watu wenyewe hasa sekta binafsi hii ina maana kuwa mahitaji ya wanawake na asasi za kijamii yanazingatiwa.

## 2.0 Nini maana ya Soko la Pamoja?

Soko la Pamoja ni soko moja la ndani ambalo linahusisha uhuru wa mzunguko wa bidhaa, uhuru wa mzunguko wa ajira, huduma na mitaji, na haki ya kuanzisha makazi na kuishi. Soko la Pamoja likishakamilika linaweza kuimarisha biashara na uwekezaji na kuifanya kanda hii kuwa na mafanikio katika uzalishaji na kupata maendeleo.

## 3.0 Soko la Pamoja lina Lengo gani?

Aya ya 1 ya Ibara ya 4 ya Itifaki inaonyesha kuwa lengo kuu la Soko la Pamoja ni kupanua na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa Mataifa Wanachama kwenye masuala ya kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya Mataifa Wanachama

## 4.0 Ni yapi malengo mahususi ya Soko la Pamoja?

**Aya ya 2 ya Ibara ya 4 ya Itifaki inaonyesha malengo mahususi ya Soko la Pamoja kuwa ni:**

- Kusukuma mbele ukuaji wa kiuchumi na maendeleo ya mataifa wanachama kwa njia ya uwepo wa uhuru wa mzunguko wa bidhaa, watu na ajira, haki ya kuanzisha makazi na kuishi na uhuru wa mzunguko wa huduma na mtaji;
- Kuendeleza upanuzi na mtangamano wa shughuli za kiuchumi ndani ya Jumuiya, na faida itakayopatikana igawanywe kwa usawa miongoni mwa mataifa wanachama na raia wake;
- Kuhamasisha uelewa wa pamoja na ushirikiano baina ya wananchi wa Nchi Wanachama kwaajili maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii;
- Kuimarisha maendeleo ya utafiti na teknolojia kwa lengo la kusukuma mbele maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii. Wanawake wanaoshiriki kwenye nyanja hizi na kwenye biashara isiyo rasmi ya kuvuka mipaka wanayo nafasi ya kunufaika kutokana na mafanikio ya malengo haya.

## 5.0 Ni zipi Sehemu za Itifaki?

Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki imegawanyika katika sehemu kadhaa kama ifuatavyo:

**Sehemu A:** Tafsiri (Sehemu hii inatoa tafsiri ya maneno kadhaa yaliyotumika kwenye Itifaki)

**Sehemu B:** Uanzishwaji wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki (Sehemu hii inatoa maelezo ya Ibara zinazoongelea uanzishwaji wa Soko la Pamoja, kanuni, malengo, na maeneo la ushirikiano kwenye Soko la Pamoja).

**Sehemu C:** Uhuru wa mzunguko wa bidhaa (Sehemu hii inaeleza masuala ya uhuru wa mzunguko wa bidhaa kwa kusimamiwa na sheria ya ushuru wa forodha ya Jumuiya kama ilivyoelezwa kwenye ibara ya 39 ya Itifaki ya uanzishwaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki).

**Sehemu D:** Uhuru wa kwenda popote na wa ajira (Sehemu hii ya Ibara inaeleza suala la uhuru wa watu kwenda popote ndani ya Jumuiya, mfumo wa utambulishaji, nyaraka za safari, uhuru wa watu kufanya kazi popote, usawazishaji na utambuzi wa pamoja wa sifa za kitaaluma na fani, na usawazishaji wa sera za ajira, sheria na programu).

**Sehemu E**: Haki ya kuanzisha makazi na kuishi (Sehemu hii ya Ibara inaeleza juu ya haki ya kuanzisha makazi, haki ya kuishi popote, na haki ya kupata na kutumia ardhi na majengo).

**Sehemu F**: Mzunguko huru wa huduma (Sehemu hii ya Ibara juu inaeleza ya mzunguko huru wa huduma inahusu huduma kwa wananchi, huduma zinazopendelewa zaidi kwa wananchi, utoaji wa taarifa, sheria za ndani, isipokuwa sababu za kipekee katika biashara ya huduma, upekee wa kiusalama kwenye biashara ya huduma, na utekelezaji wa mzunguko huru wa huduma).

**Sehemu G**: Mzunguko huru wa mtaji (Sehemu hii ya Ibara inaeleza juu ya uondoaji wa vikwazo vinavyozuia mzunguko huru wa mtaji, isipokuwa ulinzi wa biashara, masharti ya kuomba kupatiwa ulinzi wa kibiashara, na mtaji na malipo yanayohusiana pamoja na usafirishaji wa mitaji).

**Sehemu H**: Maeneo mengine ya ushirikiano katika Soko la Pamoja (Sehemu hii ya Ibara inaelezea juu ya kulinda uwekezaji uliovuka mipaka, uratibu wa kiuchumi na kifedha, usawazishaji wa sera na sheria za kodi, biashara zilizokatazwa, ruzuku zilizokatazwa, manunuzi ya umma, usalama wa mlaji, uratibu wa mahusiano ya kibiashara, uratibu wa sera za usafirishaji, usawazishaji wa sera za kijamii, usimamizi wa mazingira, ushirikiano wa kitakwimun maendeleo ya utafiti na teknolojia, ushirikiano wa hataza na haki ya ubunifu, ushirikiano kwenye maendeleo ya viwanda, na ushirikiano kwenye kilimo na usalama wa chakula).

**Sehemu I**: Vipengele vya Jumla (Sehemu hii ya Ibara inaeleza kuhusu mfumo wa kitaasisi, makadirio na usawazishaji wa sera, sheria na mifumo; hatua za kulinda biashara, hatua za kutatua ukosefu wa uwiano wa kibiashara, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Soko la Pamoja; kanuni, miongozo na maamuzi; kiambatisho; marekebisho ya Itifaki; utatuzi wa migogoro; kuanzisha na kuhifadhi na kusajili).

## 6.0 Ipi ni fasiri ya baadhi ya Sehemu za Itifaki?

Sehemu zifuatazo zimefasiriwa kama ifuatavyo:

### SEHEMU A: Tafsiri

Ibara ya 1 inatoa ufafanuzi wa istilahi zilizotumika kwenye Itifaki. Itifaki inafafanua baadhi ya istilahi za kwenye biashara kama vile: Nyaraka za pamoja za kusafiria, raia, ushirikiano na shughuli za kiuchumi na mengineyo.

**SEHEMU B: Uanzishwaji wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**Aya ya 1 ya Ibara ya 2** ya Itifaki inaonyesha kuwa ili kuhamasisha malengo ya Jumuiya yaliyotolewa kwenye ibara ya 5 ya Mkataba na kwa mujibu wa maelezo ya Itifaki, Nchi Wanachama wanaanzisha Soko la Pamoja kama sehemu muhimu ya Jumuiya.

**Aya ya 1 ya Ibara ya 3** ya Itifaki inaonyesha kuwa Soko la Pamoja litasimamiwa na kanuni za msingi na za utekelezaji za Jumuiya kama zilivyoainishwa kwenye Ibara za 6 na 7 za Mkataba.

**Aya ya 2 ya Ibara ya 3** ya Itifaki inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zizingatie kanuni ya kutobagua wananchi wa Nchi Wanachama kwa misingi ya utaifa wao; zinapaswa kuwajali wananchi wa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya, pasipo kuwaona wananchi wa nchi kama wahusika wa mbali; kuhakikisha kuna uwazi katika masuala yanayohusu nchi nyingine wanachama; na kushirikiana taarifa kwaajili ya utekelezaji wa itifaki.

**Aya ya 1 ya Ibara ya 5** ya Itifaki inaonyesha eneo la ushirikiano litahusisha shughuli yoyote itakayofanywa kwa ushirikiano kati ya Nchi Wanachama kwa lengo la kuwa na mzunguko huru wa bidhaa, watu, ajira, huduma na mtaji na kuhakikisha kuwa wananchi wanafurahia haki kuanzisha makazi na kuishi popote ndani ya Jumuiya.

**SEHEMU C: Mzunguko huru wa bidhaa**

**Ibara ya 6** inaelezea juu ya mzunguko huru wa bidhaa unaohusisha uhuru wa kusafirisha bidhaa kwa kuondoa vikwazo ili kuwepo biashara huru. Hili limefafanuliwa vizuri kwenye Itifaki ya Umoja wa Forodha kwakuwa Itifaki ya Soko la Pamoja inajumuisha Umoja wa Forodha pamoja na Itifaki nyingine tatu zinazohusu uhuru na mbili zinazohusu haki.
SEHEMU D: Mzunguko huru wa watu na wafanyakazi

**Ibara ya 7 – 12** zinaongelea juu ya mzunguko huru wa watu na wafanyakazi kwenye Nchi Wanachama. Zinahakikisha kuwa wananchi wa Nchi Wanachama wanakuwa huru kufanya kazi na kwenda kokote katika Nchi Mwanachama; kutobagua watu wanaotoka nchi nyingine, ndani ya Nchi Wanachama; wafanyakazi wanazo haki za kuthaminiwa kama wananchi wengine katika suala la ajira, marupurupu, uhuru wa kujiunga na vyama na kujumuika pamoja katika kudai haki; na kupata huduma za hifadhi ya jamii; na haki za kazi. Mfanyakazi ana haki ya kuandamana na mwenza na watoto. Mtoto anayeandama na mfanyakazi atakuwa na haki ya kuajiriwa kama mfanyakazi au kujihusisha na shughuli ya kiuchumi kwa kujiajiri kwenye nchi aliko kwa kuzingatia sheria za nchi ile anakoishi kwa kuzingatia umri unaoruhusiwa na sheria za Nchi Wanachama. Mzunguko huru wa watu utatekelezwa kwa kuzingatia mipaka ya kila Nchi Wanachama.

**Ibara ya 8** inaonyesha kuwa raia wa Nchi Wanachama lazima wawe na nyaraka za utambulisho wa utaifa wao ndani ya Jumuiya.

**Ibara ya 12** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zinapaswa kuoanisha sera zao za ajira, sheria za nchi na programu kwaajili ya kuwezesha uwepo wa uhuru wa wafanyakazi kufanya kazi kokote ndani ya Jumuiya. Uhuru wa mzunguko wa wafanyakazi ni hali ya kuendelea. Makundi tofauti ya wafanyakazi yataruhusiwa kuhama kwa nyakati tofauti kwa mujibu wa mpangilio uliowekwa kama kiambatisho iliyopo kwenye Itifaki inavyoonyesha.

**SEHEMU E: Haki ya kuanzisha makazi na kuishi**

**Ibara ya 13** inaeleza juu ya haki ya kuanzisha makazi ni ya kila mwananchi wa Nchi Wanachama na kuwa kila mwanachama ana haki ya kufanya shughuli yoyote ya kiuchumi kwa njia ya kujiajiri, kuanzisha na kusimamia shughuli za kiuchumi katika taifa jingine la Nchi Wanachama na kujiunga na mifuko ya hifadhi ya kijamii ya Nchi Wanachama kwa kuzingatia sheria za Taifa Mwanachama. Mtu anatakiwa kusajili biashara, kuwa na ofisi iliyosajiliwa na kufanya shughuli husika za kiuchumi katika nchi husika kwa kufuata sheria za ile nchi. Haki hii inayapa makampuni katika nchi ngeni kutambuliwa kama makampuni ya wenyeji na kuruhusu kuhamishwa kwa watendaji wakuu wa kampuni na wafanyakazi wa ngazi ya juu wa kampuni. Hii inamaanisha kuwa makampuni yaliyoanzishwa na wananchi wa Afrika Mashariki watasimamiwa na sheria sawa katika nchi zote za Jumuiya.

**Ibara ya 14** inaeleza juu ya haki ya ukaaji kwa yule aliyeajiriwa au aliyejiajiri katika Nchi Mwanachama, na haki hiyo inawagusa pia wenzi, watoto na wategemezi. Inahakikisha kuwa haki ya ukaaji kwa raia wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inawahusu wote waliopo katika taifa jingine la wanachama au wakiwa kama wafanyabiashara au waliofungua biashara. Masuala yanayohusu ukaazi wa kudumu bado yanasimamiwa na serikali kwa kuzingatia sera za kitaifa na sheria za Nchi Mwanachama.

**Ibara ya 15** inaeleza kuhusu upatikanaji na matumizi ya ardhi vinasimamiwa na sera na sheria za Nchi Wanachama.

**SEHEMU F: Mzunguko huru wa Huduma**

**Ibara 16 – 23** zinatambua haki ya mzunguko huru wa huduma kule ambako watoa huduma wanaweza kuzitoa huduma hizo kwa wateja na zinatolewa sawa na watoaji wa ndani katika masoko ya ndani ya Nchi Wanachama. Huduma zinazoweza kutolewa ni kama vile mawasiliano ya simu au kwa njia ya biashara kwenye Nchi Wanachama. Wanawake wajasiriamali wadogo nao pia wanahusika na uhuru huu.

Upo uhakika wa kuwa na mzunguko huru wa huduma zitolwazo na wananchi wa Nchi Wanachama na mzunguko huru wa huduma kutoka kwa wananchi wa nchi nyingine wanachama ndani ya Jumuiya. Hakuna ubaguzi dhidi ya wasambazaji, bidhaa au huduma kutoka nchi nyingine wanachama, hii inalenga kuwa na manufaa yatokanayo na ushindani huru.

**Ibara ya 19** inazitaka Nchi Wanachama kutoa taarifa kwa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusiana na makubaliano yoyote yatakayoathiri biashara ya huduma na wanachama wengine.

**Ibara ya 21** inatambua kuwa yapo masuala ya kipekee yanayohusu biashara ya huduma kwa lengo la kulinda maadili ya umma, kuwalinda wanadamu, vitendo vya utapeli wa pesa na kulinda usiri wa watu binafsi. Ni muhimu kufahamu kuwa si sekta zote za huduma zimefanywa kuwa huru. Kuyafanya mambo kuwa huru ni mchakato endelevu na utafuata mpangilio kama ulivyoonyeshwa kwenye kiambatisho za Itifaki.

**SEHEMU G: Mzunguko huru wa mtaji**

**Ibara ya 24-28** zinatoa uhuru wa mzunguko wa mtaji kwaajili ya mzunguko huru wa pesa kwa ajili ya kulipia bidhaa na huduma kutoka Nchi Wanachama; kuondoa vizuizi vya mabadilishano ya fedha za kigeni; kuhamasisha ubadilishanaji wa pesa na uwezo wa kubadilishan sarafu za nchi moja na nyingine kwa uhuru kati ya Nchi Wanachama.

**Ibara ya 25** inaeleza juu ya mazingira ambayo kutakuwepo na udhibiti wa mzunguko wa mtaji baada ya kuwepo na sababu za msingi zinazoendana na sera ya umma, utakasaji wa fedha na vizuizi vya masuala ya fedha kadiri ya makubaliano ya Nchi Wanachama.

**Ibara ya 26** inaeleza juu ya hatua za kulinda biashara kwaajili ya masoko ya fedha kwenye Nchi Wanachama.

**SEHEMU H: Maeneo mengine ya ushirikiano kwenye Soko la Pamoja**
Ibara ya 29 inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zitachukua hatua ya kulinda uwekezaji unaovuka mipaka na mapato ya uwekezaji wa Nchi Wanachama ndani ya himaya zao. Nchi zinatakiwa kutowabagua wawekezaji, kuweka ulinzi kwa wafanyabiashara wenye mitaji inayovuka mipaka ndani ya Jumuiya.

**Ibara ya 30 na 31** inaeleza juu ya haja ya Nchi Wanachama kuoanisha sera zao za uchumi na fedha ikiwemo sekta ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na ukuaji endelevu wa uchumi na maendeleo ya kiuchumi.

**Ibara ya 32** inazitaka Nchi Wanachama kuratibu na kuendelea kuoanisha sera na sheria zao za kodi ili kuondoa usumbufu wa masuala ya kodi kwa lengo la kuwezesha mzunguko huru wa bidhaa, huduma na mtaji.

**Ibara ya 33** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zitazuia vitendo vyote vibaya vinayoathiri biashara kwa kiasi kikubwa.

**Ibara ya 34** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama hazitatoa ruzuku kwa kupitia rasilimali ambazo zitaathiri au kutishia ustawi wa ushindani kwenye biashara ndani ya kanda hii.

**Ibara ya 35** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama hazitawabagua wasambazaji, bidhaa au huduma kutoka nchi nyingine ambazo ni wanachama wa jumuiya na kuacha kuzuia ushindani huru kwenye masuala ya manunuzi ya umma.

**Ibara ya 36** inaeleza kwamba Nchi Wanachama zitahamasisha maslahi ya walaji ndani ya Jumuiya kwa kuhakikisha kuwa maisha yao, afya na usalama vinalindwa na kuhamasisha ushindani wenye tija.

**Ibara ya 37** inaeleza juu ya Nchi Wanachama kuratibu mahusiano ya kibiashara baina yao na kuhamasisha biashara ya kimataifa kwa kupitisha mbinu za pamoja zinazohusiana na viwango vya ushuru, makubaliano ya kibiashara, kuwa na uwiano sawa wa kufikia uhuru wa kibiashara na kuhamasisha biashara ya nje.

**Ibara ya 38** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zitatakiwa kuratibu na kuoanisha sera za usafiri kwaajili ya kuwa na miundombinu na huduma bora inayojitosheleza, ya uhakika, salama na yenye ushindani kimataifa (barabara, reli, mito, bahari, bomba na njia nyingine kama vile bandari, viwanja vya ndege na bandari kavu).

**Ibara ya 39** inaeleza kwamba Nchi Wanachama zitaratibu na kuoanisha sera zao za ki-jamii kwaajili ya kuhamasisha na kulinda kazi zenye staha kwa lengo la kuleta maisha bora kwa raia wa Nchi Wanachama. Zitahamasisha utawala bora, utawala wa sheria na haki za kijamii, kulinda haki za binadamu, usawa wa kijinsia, kulinda haki za makundi maalumu na makundi yaliyoko kwenye mazingira magumu, kuhamasisha umoja na mshikamano miongoni mwa watu waliomo ndani ya Jumuiya.

Pia Nchi Wanachama zitatekeleza programu za kubuni ajira, kuboresha sheria za kazi na kuboresha mazingira ya kazi, kuhamasisha usalama na afya mahali pa kazi, kupiga viota ajira kwa watoto, kuhamasisha elimu rasmi, mafunzo ua ufundi stadi na ufundi mchundo, kuhamasisha haki za watu wenye ulemavu. Nchi Wanachama zinapaswa kupambana na VVU/UKIMWI, malaria na kifua kikuu, kuzuia na kupambana na magonjwa ya milipuko na magonjwa mengine, kuzuia tabia hatarishi kama vile ulevi, dawa za kulevya, kuzuia biashara haramu ya watu na usafirishaji wa binadamu.

**Ibara ya 40** inaeleza juu ya haja ya Nchi Wanachama kuhakikisha kuwa zipo kanuni madhubuti za usimamizi wa mazingira na maliasili kwaajili ya ufanisi wa Soko la Pamoja na sheria nyingine mathalani Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira na Maliasili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Itifaki ya Maendeleo Endelevu ya Bonde la Ziwa Viktoria na nyinginezo.

**Ibara ya 41:** Nchi Wanachama zitashirikiana kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi, zinazopatikana kwa wakati na za uhakika kwaajili ya kuainisha, kufuatilia na kutathmini masuala yote ya Soko la Pamoja kwaajili ya kufanya maamuzi.

**Ibara ya 42:** Nchi Wanachama zitahamasisha maendeleo ya utafiti na teknolojia kwa njia ya utafiti wenye tija ya kimasoko, maendeleo ya teknolojia na kuanzisha teknolojia kwa lengo la kuwa na uzalishaji endelevu wa bidhaa na huduma kwaajili ya ushindani wa kibiashara. Hii itahamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za kiutafiti za kikanda na kubadilishana teknolojia. Baraza la Mawaziri litatoa miongozo na kuweka kanuni kwaajili ya kuhamasisha usirikiano kwenye utafiti, maendeleo ya teknolojia na kuhamisha teknolojia. Kuanzisha mfuko wa maendeleo ya utafiti na teknolojia ambao utasaidia kusimamia mifumo ya ubunifu wa kiteknolojia.

**Ibara ya 43:** Nchi Wanachama zitashirikiana, kuhamasisha na kulinda haki za ubinifu ambazo miongoni mwa hizo ni haki miliki, hataza, aina mpya za mipango, biashara na nembo za huduma, siri za kibiashara, kielelezo cha matumizi.

**Ibara ya 44:** Nchi Wanachama zitashirikiana katika sekta ya viwanda kwa masuala yanayohusiana na uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa lengo la kufikia ukuaji endelevu na maendeleo ndani ya Jumuiya. Kwa kuwa na mfumo wa maingiliano, nchi zitahamasisha ongezeko la thamani kwenye bidhaa na mtawanyiko wa bidhaa kwaajili ya kuboresha matumizi ya rasilimali.

**Ibara ya 45:** Nchi Wanachama zitachukua hatua ya kuwa na maendeleo endelevu na kuhamasisha kilimo hususani mazao, wanyama, samaki, misitu na mazao yake na kuhakikisha kuwa kuna usalama wa chakula kwenye Jumuiya kwa njia ya upatikanaji wa chakula bora na cha kutosha kwa kuongeza uzalishaji kwenye kilimo ili pawepo na usalama wa chakula na lishe.

**SEHEMU I: Vipengele vya Jumla**

**Ibara ya 46**: Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki wanaweza kuanzisha na kuwapa mamlaka na madaraka kwa taasisi yoyote kama itafaa kufanya hivyo kwaijili ya kusimamia Soko la Pamoja.

**Ibara ya 47:** Nchi Wanachama zitasawazisha sera zao na mifumo, kwa lengo la kutekeleza Itifaki hii.

**Ibara ya 48:** Nchi Wanachama zimekubaliana kutumia mbinu za kulinda biashara wakati wa uharibifu au tishio kwa uchumi wa Nchi Wanachama baada ya kutumia vipengele sahihi vya Itifaki. Kwa upande wa suala la tishio la uharibifu, Nchi Wanachama zitawasiliana na Baraza la Mawaziri kabla ya kuchukua hatua za kulinda biashara.

**Ibara ya 49:** Baraza litakuwa na wajibu wa kuidhinisha hatua za kushughulikia tatizo la kukosekana kwa uwiano kutakakosababishwa na utekelezaji wa Itifaki hii.

**Ibara ya 50**: Baraza litaanzisha mfumo wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa itifaki hii kwa njia ya mapitio ya kila mwaka, mapitio.

**Ibara ya 51**: Mara kwa mara, Baraza litaweka kanuni, kutoa miongozo na kufanya maamuzi kwaajili ya utekelezaji wenye ufanisi wa vipengele vya Itifaki hii.

**Ibara ya 52**: Nchi Wanachama zitafikia uamuzi kuwa kiambatisho kwenye Itifaki hii kitakuwa cha lazima na kiambatisho hicho kitakuwa sehemu ya Itifaki.

**Ibara ya 53**: Itifaki hii inaweza kufanyiwa marekebisho na Nchi Wanachama kwa mujibu wa vipengele vya Ibara ya 150 ya Mkataba.

**Ibara ya 54**: Mgogoro wowote baina ya Nchi Wanachama utakaotokana na tafsiri au matumizi ya Itifaki hii utatatuliwa kwa kuzingatia vipengele vya Mkataba. Hili litafanyika kwa mujibu wa katiba zao, sheria za nchi na taratibu za kiutawala na vipengele vya Itifaki hii, Nchi Wanachama zinahakikisha kuwa:

**Ibara ya 55**: Itifaki itaanza kufanya kazi baada ya kuridhiwa na Nchi zote Wanachama na kuweka nyenzo za kusimamia kuridhiwa huko chini ya Katibu Mkuu.

**Ibara ya 56**: Itifaki na vyombo vyote vya kuridhia viliwekwa na Katibu Mkuu ambaye atatoa nakala halisi za vivuli vya Itifaki na vyombo vya kusimamia ridhaa kwa Nchi zote Wanachama.

## 7.0 Zipi faida za Soko la Pamoja kwa wanawake wanaofanya biashara ya ku vuka mipaka ndani ya ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

1. Uhuru wa kwenda popote kwa kuvuka mipaka ya nchi bila ya kubugudhiwa.
2. Uhakika wa kusafirisha bidhaa.
3. Kutobaguliwa ukiwa katika nchi nyingine mwanachama.
4. Kutokuwepo na umiliki wa soko kutokana na kuwepo kwa mazingira ya ushindani wa biashara.
5. Manufaa yatokanayo na wekevu wa mizani, kuongezeka kwa ushindani na gharama ndogo na kupata tija.
6. Urahisi wa malipo ya bidhaa na huduma kutoka nchi nyingine mwanachama.
7. Kuishi nchi nyingine mwanachama bila ya kubaguliwa.
8. Huduma sawa katika kuendesha biashara kwenye nchi nyingine mwanachama.
9. Uhuru zaidi wa kuchagua bidhaa.
10. Kuongezeka kwa ubunifu kwa kuanzisha bidhaa mpya.

## 8.0 Vipi ni vikwazo na masuala ambayo yamekuwa yakiweka wanawake kando kwenye biashara ya kuvuka mipaka ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki?

Aya ya 5 ya Ibara ya 7 inaonyesha kuwa uhuru wa watu kwenda popote utakuwa na mipaka itakayowekwa na nchi mwenyeji kwa misingi ya sera ya umma, usalama wa umma au afya ya watu.

Aya ya 11 ya Ibara ya 10 inaeleza juu ya uhuru wa wafanyakazi kwenda popote nao utakuwa na mipaka yake itakayowekwa na nchi mwenyeji kwa misingi ya sera ya umma, usalama wa umma au afya ya watu.

Aya ya 8 ya Ibara ya 13 inaeleza kuwa haki ya kuanzisha makazi au kuishi nayo itakuwa na mipaka yake itakayowekwa na nchi mwenyeji kwa misingi ya sera ya umma, usalama wa umma au afya ya watu.

Aya ya 1 ya Ibara ya 25 inaonyesha kuwa mzunguko huru wa mtaji unaweza ukawa na mipaka yake baada ya kuwa na sababu za msingi kama vile usimamizi wa busara, sera za umma, utakasaji wa fedha, na vikwazo vya fedha kama ilivyokubaliwa na Nchi Wanachama.
Sera ya umma inamaanisha sera za serikali au maamuzi yanayohakikisha usalama wa raia na wakaaji wa kutoka nchi nyingine, mashirika na taasisi dhidi ya vitisho kwa ustawi wao na ustawi wa jamii zao.

Usalama wa umma inamaanisha utendaji wa serikali unaohakikisha usalama wa raia na wakaaji wa kutoka nchi nyingine mashirika na taasisi dhidi ya vitisho kwa ustawi wao na ustawi wa jamii zao.

Afya ya watu inamaanisha maeneo yanayolindwa na kuhamasisha afya na ustawi na kuzuia magonjwa na kuongeza umri wa kuishi kwa serikali kuhakikisha kuwa usalama unawekwa kwa raia wake na wakaaji wa kutoka nchi nyingine, mashirika na taasisi wanalindwa dhidi ya vitisho vinavyohatarisha ustawi wao na ustawi wa jamii zao.

## 9.0 Mapendekezo

### Sera

1. Serikali ziharakishe uratibu na usawazishaji wa sheria za nchi na sera kwaajili ya utekelezaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki.
2. Serikali zitoe vitambulisho vya uraia na ukazi kwa raia wote kwaajili ya kurahisisha uhuru wa kusafiri kokote ndani ya Jumuiya.
3. Serikali ziharakishe ukamilishaji wa kiambatisho cha Itifaki ya Soko la Pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa Soko la Pamoja.
4. Serikali zigatue utoajia wa vyeti vya kuingiza bidhaa zenye thamani chini ya dola 2000 ili kuwawezesha wanawake kufanya biashara ya kuvuka mipaka.

### Mengineyo

1. **Mbali na serikali, Asasi za Kiraia na sekta binafsi zifanye kazi ya kuwaelimisha wanawake kuhusu faida na fursa zilizopo; namna ya kunufaika na kutumia fursa za Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.**
2. **Asasi za Kiraia na sekta binafsi zishiriki kwenye majadiliano juu ya kiambatisho cha Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwaajili ya utekezaji kamili wa Soko la Pamoja.**

## 10. Hitimisho

Utekelezaji wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima uendane na ushiriki ulio bora na kwa wingi wa watekelezaji wote (wanaume na wanawake), sekta zote za uchumi. Jumuiya wa wafanyabiashara kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi, mashirika ya kiraia (kama vile ajira, asasi za kirai/Asasi zisizo za serikali, asasi za kidini, makundi ya utamaduni nk) lazima yashirikishwe kikamilifu na suala la jinsia nalo lizingatiwe katika utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja katika ngazi zote.

Wafanybiashara wadogo wadogo wanawake ambao ndio wengi katika nyanja za kiuchumi na kijamii watanufaika zaidi wakionyeshwa faida na fursa zilizomo kwenye Soko la Pamoja na jitihada zichukuliwe kwa pamoja kati ya serikali na sekta binafsi zikiwemo Asasi za kiraia kwa lengo la kuboresha ushiriki wao.

# 10. VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: AINA NA VYANZO VYA NYARAKA ZINAZOTUMIKA KWENYE EAC

| Aina ya waraka | Nyaraka za muda za kusafiria | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Nchi | Uganda | Tanzania | Kenya | Rwanda | Burundi |
| Ada | UGX 5000 | TSH 10,000 | KSH 300 | Bure | N/A |
| Mahali | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote ya Uganda | Ofisi za Uhamiaji Arusha na mipakani kote | Idara ya Uhamiaji Mipakani na Makao makuu ya Uhamiaji Nairobi | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote |
| Aina ya waraka | Pasipoti ya EAC | | | | |
| Ada | UGX 52,000 | TSH 30,000 | KSH 940 | 20,000Rf | N/A |
| Mahali | Idara ya Uhamiaji makao makuu | Idara ya Uhamiaji Dar-es-saalam au Arusha | Idara ya Uhamiaji makao makuu Nai-robi, Nyayo House | Idara ya Uhamiaji makao makuu Ki-gali. | Paspoti ya Afrika Mashariki haijaanza kutumika nchini Burundi |
| Aina ya waraka | Pasipoti ka Kitaifa | | | | |
| Ada | UGX 82,000 | TSH 50,000 | KSH 3040 (for a 32 pages passport) | 50,000Rf | 135,000BF |
| Mahali | Idara ya uhamiajim katika ofisi za wilaya, Wizara ya Mabo ya ndani Idara ya pasipoti makao makuu | Ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam | Ofisi za Uhamiaji Nyayo house | Mako makuu ya Uhamiaji Kigali | Mako makuu ya Uhamiaji Bujum-bura |


| Aina ya waraka | Nyaraka za muda za kusafiria | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Nchi | Uganda | Tanzania | Kenya | Rwanda | Burundi |
| Ada | UGX 5000 | TSH 10,000 | KSH 300 | Bure | N/A |
| Mahali | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote ya Uganda | Ofisi za Uhamiaji Arusha na mipakani kote | Idara ya Uhamiaji Mipakani na Makao makuu ya Uhamiaji Nairobi | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote |
| Aina ya waraka | Pasipoti ya EAC | | | | |
| Ada | UGX 52,000 | TSH 30,000 | KSH 940 | 20,000Rf | N/A |
| Mahali | Idara ya Uhamiaji makao makuu | Idara ya Uhamiaji Dar-es-saalam au Arusha | Idara ya Uhamiaji makao makuu Nai-robi, Nyayo House | Idara ya Uhamiaji makao makuu Ki-gali. | Paspoti ya Afrika Mashariki haijaanza kutumika nchini Burundi |


**ANGALIZO: Kuna hati za nyongeza kwa bidhaa maalumu**
Kwa biashara ya wanyama, unatakiwa kuwa na kibali cha kusafirisha wanyama na biadha za wanyama na Cheti cha Afya ya Wanyama
Kwa mbwa na paka unatakiwa na kibali cha kusafirisha mbwa na paka
(Nyaraka hizi zinaweza kupatikana katika idara ya mifugo na entomolojia – Wizara ya Mifugo na Uvuvi)
**Nyingine**
Kwa vyakula na vinywaji, ni lazima uwe na cheti cha uchambuzi kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali
Kwa samaki, unatakiwa kuwa na kibali cha kusafirisha samaki na Cheti cha Afya kutoka idara ya uvuvi – Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

# KIAMBATISHO 2: HATI RAHISI YA UASILI WA BIDHAA (SSCO)



EAST AFRICAN COMMUNITY
SIMPLIFIED CERTIFICATE OF ORIGIN
(For goods of a value not exceeding US $ 500)
*(Kwa bidhaa zenye thamani isiyozidi US$ 500)*

| | |
|---|---|
| 1) Exporter (name, full address, country)<br>*Msafirishaji (Jina na anwani)* | Reference Number ..............<br>*Kumb Na* |
| 2) Importer (Names & address)<br>*Mwingizaji bidhaa, ( Jina na anwani yake)* | 3)Country of Origin<br>*Uthibitisho wa uasili wa bidhaa* |

| | | |
|---|---|---|
| 4)Description of goods<br>*Maelezo ya bidhaa* | 5)No. and type of packages<br>*Namba na aina ya kifurushi* | 6)Value<br>*Thamani* |

| | |
|---|---|
| 7)Declaration by Exporter<br>*Tamko la Msafirishaji/Mzalishaji/Mgavi*<br>I, the undersigned Mr/Mrs/Ms.......................... declare that the goods described above have been produced (country)..................in accordance with the EAC Rules of Origin.<br>Signature.......................................<br>*(Saini)*<br>Place.......................................<br>*(Mahali)*<br>Date.......................................<br>*(Tarehe)*<br>Official stamp<br>*(Mhuri)* | 8)Customs Endorsement<br>*Uthibitisho wa forodha*<br>I, the undersigned, hereby endorse the exporters' declaration and certify that the goods qualify under the EAC Rules of Origin.<br>Signature.......................................<br>*(Saini)*<br>Place.......................................<br>*(Mahali)*<br>Date.......................................<br>*(Tarehe)*<br>Official stamp<br>*(Mhuri)* |

© EASSI 2012

Haki zote zimehifadhiwa. Kuchapisha tena kitabu chote au sehemu kwa madhumuni ya kueleimisha au yasiyo ya kibiashara kunaruhusiwa lakini baada ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwenye dhamana ya haki miliki iwapo tu mtumiaji ataonyesha kwa uwazi chanzo na nyongeza au badadilisho yoyote, kama yatakayokuwepo.

*The Eastern African Sub-regional Support Initiative for the Advancement of Women (EASSI), P.O.Box 24965, Kampala, Uganda,
Tel: +256414285163/312 266 451*